



BARAZA LA DIASPORA LA WATANZANIA DUNIANI

Kumb. Na:TDC20200323/01

23.03.2020

WATANZANIA DIASPORA.
DUNIANI.

KUH: MLIPUKO WA UGONJWA WA COVID-19.

Ndugu Watanzania Diaspora,

Kama tujuavyo, ulimwengu mzima hivi sasa upo katika taharuki ya ugonjwa wa **COVID-19**. Ni ugonjwa hatari. Mbaya zaidi, tayari mwenendo wa mlipuko wa ugonjwa huu unaonyesha kuwa na madhara makubwa sio tu kijamii bali pia kiuchumi.

Uongozi wa **TDC-Global** unawaandikia kuwapa pole nyote ambao mmeathirika tayari kwa njia moja au nyingine ikiwemo kiuchumi na kijamii. Mbali ya pole na kuwatakieni kila la kheri katika kukabiliana na janga hili, tungependa kusisitiza kuhusu kusikiliza na kufuata masharti na maelekezo yanayotolewa na wataalamu na viongozi juu ya kujilinda na kulinda wengine.

Pia, katika kipindi hiki kigumu, tunawasihi muendeleo kupendana, kushirikiana na kusaidiana kwa hali na mali. Hiki ni kipindi cha kudumisha umoja na udugu wetu. Kama watanzania, tunayo sifa hiyo. Ni sifa nzuri. Tuiendeleze.

Poleni sana.

“PAMOJA TWaweza”

Wenu Mtiifu,

Norman Jasson

Mwenyekiti TDC Global

+46734974141

